

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWT/L1/53

23.05.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa kuzingatia kibali cha ajira cha tarehe **13 Mei, 2022** chenye Kumb Na. **FA.97/228/01/09** Kutoka kwa Katibu Mkuu **OR-UTUMISHI**, Anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zifuatazo:-

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III NAFASI (14)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao,kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- viii. Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mtanzania na pia awe na kita.
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita.
- iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo –Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi na asiwe na *umri unaozidi miaka 45*.
- v. Awe na afya njema, mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote katika vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

2. KATIBU MUHTASI III, NAFASI (4)

2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu kidato cha IV aliyehudhuria mafunzo katika Chuo cha Utumishi wa Umma au Chuo kinachotambulika na Serikali u Chuo na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu, awe amefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na kingereza maneno 80 kwa dakika 1 na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na serikali na kupata cheti katika programu za window Microsoft office, Excel, Internet, email na Publisher.

2.3 MAJUKUMU

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, mali, wageni, tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi ofisini
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumwalifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maafisa walio sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
- vii. Kutekeleza kazi yoyote atakayokuwa amepangiwa na msimamizi wake.

3.3 NAMNA YA KUOMBA PAMOJA NA MASHARTI YA JUMLA


- a. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Kijiji Cha Nyamwaga, Barabara ya Nyamwaga, S.L.P 16, Tarime-Mara.
- b. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya taaluma na vya mafunzo na cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.
- c. Testimonials' 'Provisional Results', Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI**
- d. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya **TCU** na **NECTA**.
- e. Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika Utumishi wa Umma wakaacha, wakastaafu, wakastaafishwa au wakafukuzwa hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- f. Vyeti vitafanyiwa uhakiki kwa kushirikiana na mamlaka husika za **NECTA**, **TCU** na Vyuo waombaji walivyosomea na endapo itagundulika mwombaji amehusisha vyeti vya kughushi kwenye maombi yake atachukuliwa hatua za kisheria.
- g. Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali **TGS 'B'**

3.1. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyamwaga, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08.06.2022** saa **9:30** alasiri.

Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ya:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 16,
TARIME.**


Peragia J. Barozi
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
TARIME**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**